# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# OFISI YA RAIS

# TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO SHULE YA SEKONDARI KISAZA -2024

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**Namba za Simu:.**

**Mkuu wa Shule 0712686385/0768864444**

**Makamu Mkuu wa Shule.0653265242**

**Mtaaluma- 0675706818**

**Matron/Patron. 0768820271**

**Shule ya Sekondari Kisaza**

**S.L.P.. 70-Handeni**

**Tarehe .......................**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi …………**

**……………………………………………..**

**S.L.P ……………………………………..**

**…………………………………………….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KISAZA HALMASHAURI YA HANDENI MKOA TANGA MWAKA 2024**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2024 na atasoma tahasusi ya CBG/HGK

Shule ya Sekondari Kisaza ipo umbali wa Kilometa 3km Kaskazini Mashariki mwa Mji wa Komkonga. Usafiri wa basi kutoka Dar-es-Salaam panda mabasi yaendayo Tanga, Arusha, Lushoto na Kilimanjaro kupitia chalinze/bagamoyo, msata, mkata shuka komkonga. Wanaotokea Arusha panda magari yaendayo Dar-es-Salaam kupitia Moshi, Korogwe, segera, kabuku shuka komkonga. Wanaotoka Dodoma/Morogoro panda magari yaendayo Tanga kupitia Chalinze, mkata shuka komkonga. Nauli kwa pikipiki kutoka kituo cha komkonga hadi shuleni Kisaza ni Tshs. 1,500/=

Muhula wa Masomo unaanza tarehe ................, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe................... Mwisho wa kuripoti ni tarehe……………….

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Sare za Shule**

- Sare ya shule hii ni suruali nyeusi mbili upana chini ni kuanzia sm 14 mpaka sm15 na marinda mawili na mashati mawili meupe kwa Wavulana.
- Sare ya Michezo ni truck suit ya blue na bukta ya blue
- Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;
- Soksi jozi mbili nyeusi za shule;
- Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali;
- Sweta moja *rangi ya blue*
- Nguo za kushindia (*shamba dress*) ni suruali mbili rangi ya kaki
- T-shirt ya blue isiyokuwa na maandishi na yenye nembo ya shule (zinapatikana shuleni).
- Tai mbili rangi nyeusi;
- Tisheti (T-shirt) rangi ya njano zenye nembo ya shule (zinapatikana shuleni).

**Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

- Madaftari nane (08) counter book quire three/four
- **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;
- Vitabu vya masomo ya tahasusi husika;
- Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology;
- Scientific Calculator;

- Godoro 2.5 ft
- Mashuka ya blue 1 na pink 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1 rangi ya blue.
- Nguo za ndani za kutosha;
- Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
- Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
- Kwanja 1, jembe 1, panga 1, softbroom 1 na hardbroom 1 na ufagio wa chelewa 1.

### 2.3 Michango mbalimbali

**a) Shule za Bweni**

| Na | Aina ya mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1 | Mchango wa uendeshaji wa shule | 65,000/= |
| 2 | tahadhari | 5,000/= |
| 3 | Nembo | 5,000/= |
| 4 | kitambulisho | 5,000/= |
| | jumla | 80,000/= |

Michango ingizwe kwenye akaunti namba **41401200045** jina la akaunti **KISAZA SEKONDARI**

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

- Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
- Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
- Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
- Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;

- Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
- Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
- Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
- Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
- Kutunza mali za shule;
- Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
- Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

- Wizi;
- Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
- Kugoma na kuhamasisha mgomo;
- Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
- Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
- Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
- Kufuga ndevu;
- Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
- Uvutaji wa sigara;
- Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
- Kupata ujauzito au kutoa mimba;
- Kusababisha mimba;

- Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
- Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
- Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
- Kudharau Bendera ya Taifa;
- Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
- Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

- Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
- Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
- Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
- Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule**

.................................................................

**IMAMU S. JUMA**
**MKUU WA SHULE**

THE HEADMASTER
KISAZA SECONDARY SCHOOL

**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- Mkuu wa shule - 0712686385
- Makamu Mkuu wa Shule - 0784715511
- Mwandamizi Taaluma - 0675706818
- Mwandamizi Malezi - 0768820271

**OFISI YA RAIS**
**LOCAL GOVERNMENT AND REGIONAL ADMINSTRATION**
**HANDENI TOWN COUNCIL**
**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

KISAZA HIGH SCHOOL,
P.O.BOX 70,
HANDENI – TANGA.

DATE:……………….

MEDICAL OFFICER,

……………………………………………

……………………………………………

……………………………………………

……………………………………………

NAME OF STUDENT

…………………………………………………………………………………………………………..

(Please examine the above named boy to ascertain her fitness for further studies)

………………………………………….

HEADMASTER

**MEDICAL CERTIFICATE.**

(To be completed by the medical officer)

I have examined the above named with regard to:-

Skin ………………………………………………………………………………………………

Eyes ……………………………………………………………………………………………

Chest ……………………………………………………………………………………………

Spleen ……………………………………………………………………………………………

Abdomen …………………………………………………………………………………………

Urine ……………………………………………………………………………………….

Stool ……………………………………………………………………………………………

Hemoglobin ………………………………………………………………………………

**And I considered:-**

1. He is good health, free from infection diseases, worms, bilharzias and fit to go to school.
2. He is now fit to return to school having treatment for

……………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………

**NAME AND SIGNATURE OF MEDICAL OFFICER** **DATE.**

And I considered:-

3. He is now fit to return to school having checked for ……………………………………………

NAME AND SIGNATURE OF MEDICAL OFFICER DATE

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA HANDENI**

KISAZA HIGH SCHOOL
S.L.P. 70,
HANDENI – TANGA.

**FOMU YA KUKUBALI NAFASI ALIYOPEWA**

**SEHEMU A.**
HABARI ZA MWANAFUNZI.

1. Jina kamili ………………………………………………………………………………………

2. Tarehe ya kuzaliwa …………………Wilaya alipozaliwa………………… Kijiji …………………

**3. Kukubali nafasi (Ijazwe na mwanafunzi)**

Mimi ……………………………………………………………………… nimeona maagizo yote ya kujiunga na shule ya sekondari ya Kisaza-Handeni na ninakubali kutimiza masharti yote ya shule ikiwa ni pamoja na uletaji wa vifaa vinavyohitajika na kutii sheria zote za shule. Nitakapokuwa shuleni Kisaza nitajitahidi kadri ya uwezo wangu kuzingatia yote ambayo wanafunzi wanatakiwa kutimiza katika suala zima la kupata Elimu ya kujitegemea.

Sahihi ya Mwanafunzi …………………………… Tarehe ……………………........

**SEHEMU B:**
**HABARI ZA MZAZI/MLEZI (IJAZWE NA MZAZI/MLEZI)**

1. Jina kamili ………………………………………………………………………………………
2. Mzazi/Mlezi ……………………………………………………………………
3. Kazi yake …………………………………………………………………………………………
4. Anwani ya Mzazi/Mlezi:…………………………………………………………………

5. Namba tatu za simu ikiwemo ya Mzazi/Mlezi na Ndugu wa karibu wa Mwanafunzi:-
   (a) ……………………………………………………………………………………………
   (b) ……………………………………………………………………………………………
   (c) ……………………………………………………………………………………………

**UTHIBITISHO:-**

Mimi Mzazi/Mlezi wa

………………………………………………………………………………………………..

nimehakikisha kwamba maagizo yote yameeleweka na mtoto wangu amejaza kikamilifu sehemu A.

Sahihi ya Mzazi/Mlezi ………………………………… Tarehe ……………………………